THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

TFN. 4
REV. 3/74

## MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY
### T1360071 - VETA PWANI RVTSC
### PAYMENT VOUCHER

Station No: ______________________

**PV No: T1360071V2200590**

| | |
|---|---|
| Payee's Name | : ASANTEEL FREDRICK MSUYA |
| Account Name | : ASANTEEL FREDRICK MSUYA - 40201604993 |
| Payee's Code | : 118-638-344 |
| Address | : PO. BOX 30090 PWANI |
| VRN | : NA |
| TIN: | : 118-638-344 |

**Payment in Respective of:**

Being supply and fixing Aluminium frames and windows

**To be Paid from:** VETA CRDB Expenditure Account

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
25 APR 2022
KIBAHA
PWANI

| | |
|---|---|
| **Apply Date** | : 25 April 2022 |
| **Reference No** | : T1360071CO2200017 |
| **Source Module** | : CONTRACT |
| **Invoice No** | : INVOICE NO. 0001 |
| **Invoice Date** | : 25 April 2022 |
| **Voucher Classificatn** | : 201 |
| **Terms of Payment** | : NA |
| **Payment Method** | : EFT |

**ACCOUNT ENTRIES**

| ACCOUNT CODE | ACCOUNT DESCRIPTION | AMOUNT |
|---|---|---|
| 046\|7002\|TR136\|313A\|E710000\|00000000\|201\|0000\|D04\|D11D03\|2\|00000\|0GT\|22019101 | Cement, Bricks and Building Materials | 49,570,000.00 |
| 7002\|TR136\|0000\|E710000\|00000000\|201\|0000\|000\|000000\|2\|00000\|000\|33182107 | WithHoldingTax | - 1,586,240.00 |

**NET AMOUNT: *******47,983,760.00**

**AUTHORITY:**

Certify that the above sum of **TZS** (in words) **FORTY-SEVEN MILLION NINE HUNDRED EIGHTY-THREE THOUSAND SEVEN HUNDRED SIXTY AND ZERO CENTS ONLY** is correctly payable to the above-named person and that the rates of payment/price(s) is/are in accordance with Regulations/the Terms of the Contract and the funds are available under the Sub-Vote and Item quoted above to meet this payment.

| | | |
|---|---|---|
| **Prepared by:** MARIAGORETH JUSTINIAN PONTIAN | **Examined by:** NITIKE ELIAH MWAMBIJE | **Approved By:** CLARA GEORGE KIBODYA |
| **Signature of Originating Officer** | **Signature of Examining Officer** | **Signature of Authorizing Officer** |
| Date: 25/04/2022 | Date: 25/04/2022 | Date: 25/04/2022 |

# THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

## PAYMENT REMITTANCE ADVICE

| | | | |
|---|---|---|---|
| TO | : ASANTEEL FREDRICK MSUYA | FROM | : VETA PWANI RVTSC |
| Payee's Code | : 118-638-344 | Payer's Code | : T1360071 |
| Bank Name | : NATIONAL MICROFINANCE BANK LIMITED | Payer's Account | : 0150590545500 - DEVELOPMENT |
| Bank Account | : 40201604993 | Account Name | : VETA CRDB Expenditure Account |
| BIC | : NMIBTZTZ | Payer's Address | : PWANI, Pwani Region |

**The following payment has been remitted**

| | |
|---|---|
| **Payment Reference Number** | : T1360071V2200590 |
| **Payment Document Number** | : T1360071D2200463 |
| **Payment Date** | : 28 Apr 2022 |
| **Payment Settlement Status** | : SETTLED THROUGH TISS ON 2022-04-29 WITH BANKING REFERENCE FP06931BB99BB8D3 |
| **Payment Currency** | : TZS |
| **Payment Amount** | : 47,983,760.00 |
| **Control Number** | : NA |

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
25 APR 2022
KIBAHA PWANI

### Remittance Detail

| INVOICE NUMBER | INVOICE DATE | LEGAL NUMBER | PAYMENT METHOD | PAYMENT DESCRIPTION | AMOUNT PAID |
|---|---|---|---|---|---|
| INVOICE NO. 0001 | 25 Apr 2022 | T1360071V2200590 | EFT | Being supply and fixing Aluminium frames and windows | 47,983,760.00 |

**PRINTED BY:**

SIGNATURE: [signature]

NAME: MARIAGORETH JUSTINIAN

# MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

## MKATABA WA KUUZA, KUTENGENEZA NA KUWEKA FLEMU NA MADIRISHA YA ALUMINIUM KATIKA MRADI WA CHUO CHA UFUNDI WILAYA YA RUFIJI (RUFIJI DVTC)

## MKATABA NA PA/024/2021/22/RUF/DVTC/ALM/01

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe **14** mwezi **04 - 2022**

**KATI YA**

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha **PWANI, S.L.P. 30345, KIBAHA, PWANI** ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

**NA**

**M/S ASANTEEL FREDRICK MSUYA wa S. L. P.30090 KIBAHA PWANI.** (ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Mzabuni wa kuuza,kutengeneza na kuweka flemu na madirisha ya aluminium ") kwa upande mwingine.

VOCATIONAL TRAINING SERVICE CENTRE REGIONAL PAID 25 APR 2022 KIBAHA PWANI

**KWA KUWA** Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

**KWA KUWA** Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya RUFIJI;

**KWA KUWA** Mwajiri amefanya majadiliano na Mzabuni wa kuuza,kutengeneza na kuweka madirisha na flemu za aluminium kwa ajili ya mradi wa Chuo cha VETA Wilaya ya RUFIJI.

**HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:**

1. **GHARAMA ZA KAZI YOTE KWA UJUMLA**

   Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania **90,200,000/=** kwa kazi ya kununua,kutengeneza na kuweka madirisha ya aluminium kama inavyoonekana kwenye jedwari hapo chini kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.

   Katika Mkataba huu,kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama za kuuza,kutengeneza na kuweka flemu na madirisha ya aluminium"

Gharama za kazi zitakazofanyika katika kila jengo ni kama ifuatavyo:

| S/N | | JENGO | BEI ILIYOKUBALIKA |
|---|---|---|---|
| | | **KUUZA,KUTENGENEZA NA KUWEKA FLEMU NA MADIRISHA YA ALUMINIUM KAMA INAVYOSOMEKA KWENYE MICHORO NA KWENYE KOTESHENI** | |
| 1 | | UTAWALA | 22,300,000 |
| 2 | | NYUMBA YA MKUU WA CHUO | 5,700,000 |
| 3 | | NYUMBA YA WAFANYAKAZI | 9,600,000 |
| 4 | | BWENI-WAVULANA | 16,750,000 |
| 5 | | BWENI WASICHANA | 17,650,000 |
| 6 | | VYOO (WASICHANA,WAVULANA, WAFANYAKAZI) | 6,300,000 |
| 7 | | STOO KUU | 1,250,000 |
| 8 | | KIBANDA CHA MLINZI | 850,000 |
| 9 | | UHAZILI NA KOMPYUTA | 9,800,000 |
| | | **JUMLA** | **90,200,000** |

## 2. MABADILIKO YA GHARAMA YA KAZI (*MATERIALS COST ADJUSTMENT*)

Gharama za kazi hazitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko yoyote yaliyofanywa na Mwajiri.

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
25 APR 2022
KIBAHA PWANI

## 3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO

Malipo yatafanyika aidha baada kazi yote kukamilika au baada ya kufikia asilimia kadhaa kama ilivyoainishwa katika mkataba huu.

(a) Malipo ya awali 10% ya gharama ya kazi
(b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya kazi;
(c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya kazi;
(d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya kazi;
(e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya kazi.

## 4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI

(a) Mzabuni atakabidhi kazi kwa wahusika wakuu waliopo eneo la ujenzi na kusainisha hati za mapokezi na nyaraka zingine muhimu kuonesha ukamilishaji wa kazi..

(b) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Mzabuni i kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo pasipo kuathiri pande zote.

## 5. WAJIBU WA MZABUNI

Mzabuni atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kutengeneza flemu na madirisha ya aluminium kwa kadri alivyokubaliana katika mkataba sambamba na maelekezo ya Mwajiri.

(b) Kumjulisha Mwajiri kuhusu mapungufu au mkanganyiko wowote utakaobainika

Katika kazi hiyo.

(c) Kuhakikisha usalama wa kazi katika eneo la ujenzi.

(d) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi unayoifanya

(e) Kukubali kukatwa na Mwajiri kodi ya zuio (withholding tax).

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
25 APR 2022
KIBAHA PWANI

## 6. WAJIBU WA MWAJIRI

Mwajiri atakuwa na wajibu ufuatao: -

(a) Kumlipa Mzabuni malipo halali ya kazi iliyoainishwa katika Mkataba huu kulingana na utaratibu uliobainishwa katka kipengele Na.3 cha Mkataba huu, pale Mzabuni atakapokuwa ametimiza wajibu wake kikamilifu kulingana na Mkataba huu.

(b) Kutoa idhini/kibali cha kuanza kazi kwa mzabuni

(f) Kuzingatia na kutekeleza masharti yote ya Sheria za nchi zinazohusiana na kazi husika.

(c) Kumkata Mzabuni kodi ya zuio (withholding tax).

## 7. MSIMAMIZI WA UJENZI (PROJECT SUPERVISOR)

(a) Mwajiri atakuwa na haki ya kuweka Msimamizi wa Ujenzi (*Site Supervisor*), ambaye atakuwa na jukumu la kufanya uhakiki wa shughuli za ujenzi,kupokea vifaa vya ujenzi akisaidiana na kamati ya mapokezi kwa niaba ya Mwajiri, na Mzabuni atatoa ushirikiano wote kwa Msimamizi wa Ujenzi (*Project Supervisor*) au Mwakilishi wake katika kutimiza majukumu yake.

(b) Msimamizi wa Ujenzi (*Site Supervisor*) akisaidiana na Mtunza Stoo ndio watakuwa wapokeaji wakuu wa vifaa vya ujenzi husika.Mzabuni anapaswa kuonana na wahusika hao kwa taratibu zote za kukabidhiana vifaa hivyo.

## 8. NOTISI *(NOTICES)*

Mawasiliano yote, Hati, Notisi yatakayofanyika katika Mkabata huu, yatafanyika kwa ama kupelekwa moja kwa moja(physically) kwa upande wowote wa Mkataba au kupitia anwani ya posta kwa barua iliyosajiliwa (registered mail).

## 9. SHERIA ZINAZOTUMIKA

Sheria za kutafsiri Mkataba huu na ufanyaji wa kazi katika Mkataba huu ni Sheria za Tanzania.

## 10. RUSHWA

Iwapo Mzabuni wa usafirishaji vifaa vya ujenzi, watumishi au wasaidizi wake katika kutekeleza majukumu haya kama kujihusisha na masuala yoyote ya rushwa ama jinai yoyote, basi Mwajiri anaweza kuvunja Mkataba huu.

## 11. KUVUNJWA KWA MKATABA

Mkataba huu unaweza kuvunjwa na upande wowote wa Mkataba huu.

(a) Mkataba kuvunjwa na Mwajiri:
Bila ya kuathiri haki zozote za Mwajiri, iwapo Mzabuni w akifanya makosa yafuatayo:

i. Kutofanya kazi kazi kwa kiwango kilichotakia

ii. kutofuata maelekezo sahihi ya Mwajiri

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
25 APR 2022
KIBAHA PWANI

## 12. USIRI

Nyaraka zote zitakazotumika katika Mkataba huu hazitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa kazi unayohusu Mkataba huu. Pia taarifa yoyote itakayopatikana wakati wa kazi inayohusu Mkataba huu haitatumika kwa madhumuni mengine yoyote isipokuwa kwa kazi inayohusu Mkataba huu.

## 13. USULUHISHI WA MIGOGORO

Mgogoro wowote utakaotokana na utekelezwaji wa Mkataba huu au baada ya utekelezwaji wa Mkataba utasuluhishwa kwa majadiliano ya pande zote za Mkataba. Iwapo majadiliano yatashindwa kusuluhisha mgogoro, basi upande wowote utatoa Notisi ya siku kumi na nne ya kuupeleka mgogoro usuluhishi kwa njia ya usuluhishi(arbitration).

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA PWANI (PWANI RVTSC)

Jina: CLARA KIBODYA Saini: [signature]

Wadhifa: KAIMU MKUU WA CHUO Tarehe: 14/04/2022

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: LUKA C. MKINI Saini: [signature]

Wadhifa: M/KITI KAMATI YA UJENZI Tarehe: 14/04/2022

REGIONAL VOCATIONAL TRAINING & SERVICE CENTRE
PAID
25 APR 2022
KIBAHA
PWANI

**IMESAINIWA NA MZABUNI**

Mbele ya

Jina: ASANTEEL FREDRICK MSUYA Saini: [signature]

Wadhifa: MKURUGENZI Tarehe: 14/04/2022

ASANTEEL FREDRICK MSUYA
P.O. Box 30091 KIBAHA PWANI
Dealers: aluminium works
TIN: 148-638-344

**Mbele ya (Shahidi)**

Jina: HAJI A. MSUYA Saini: H.MSUYA

Wadhifa: FUNDI MKUU Tarehe: 14/04/2022